HOTUBA YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA KIKAO CHA KAMATI YA AFYA MSINGI KUHUSU KAMPENI YA CHANJO DHIDI YA UGONJWA WA POLIO KWA WATOTO TAREHE 11 SEPTEMBA, 2023.

- ***Katibu Tawala Mkoa wa Rukwa,***
- ***Kamati ya Usalama Mkoa,***
- ***Wahe. Wakuu wa Wilaya (Sumbawanga, Kalambo na Nkasi),***
- ***Wakuu wa Seksheni na Vitengo,***
- ***Wakurugenzi wa Halmashauri,***
- ***Wawakilishi toka Wizara ya Afya,***
- ***Wawakilishi toka TAMISEMI,***
- ***Waganga Wakuu wa Halmashauri,***
- ***Viongozi wa Dini,***
- ***Machifu,***
- ***Waandishi wa Habari,***
- ***Wageni waalikwa,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…….

Awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sisi sote kukutana mahali hapa tukiwa wazima na wenye Afya njema, Kipekee niwakaribishe Mkoani kwetu Wajumbe wote waliotoka nje ya Mkoa wetu wa Rukwa. Karibuni sana. Aidha nimshukuru sana Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan , Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kujali Afya ya Mama na Mtoto

tangu aingie Madarakani hasa katika utoaji wa Chanjo mbalimbali kwa Watoto na ujenzi wa Miundombinu ya huduma za Mama na Mtoto.

Ndugu Washiriki, Mtakumbuka kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) mfululizo, nchi yetu kama ilivyo kwa Mataifa mengine ilikabiliana na janga la ugonjwa wa UVIKO-19 ambao umeleta athari kadhaa kwa afua nyingine za afya ikiwemo kuathiri mwitikio wa chanjo mbalimbali nchini. Mathalani, kwa mwaka 2020 hadi mwaka 2022, kwa Mkoa wa Rukwa jumla ya watoto 60,879 hawakukamilisha ratiba za chanjo mbalimbali. Hali hii imepelekea kuanza kujitokeza kwa visa na milipuko ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo ambayo yalikuwa yamedhibitiwa ikiwemo ugonjwa wa Surua na Polio.

Kwa mara ya mwisho, mgonjwa wa Polio nchini aligundulika mwaka 1996. Hivyo, Shirika la Afya Duniani (WHO) liliitangaza Tanzania kuwa nchi isiyo na maambukizi ya ugonjwa wa Polio mnamo mwezi Novemba, 2015.

Ndugu Washiriki, Mnamo tarehe 26 Mei, 2023, Wizara ilipokea taarifa za uwepo wa mtoto mmoja mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi kumi na moja ambaye alionyesha dalili za kupooza kwa ghafla. Mtoto huyu alitolewa taarifa kutoka Manispaa ya Sumbawanga, hapa Mkoani Rukwa. Uchunguzi wa Maabara ulithibitisha kuwa mtoto huyo alikuwa na maambukizi ya virusi vya Polio.

Ndugu Washiriki, Maambukizi ya virusi vinavyosababisha ugonjwa wa Polio yametolewa taarifa katika nchi zinazopakana nasi kama Burundi, Congo (DRC) na Zambia. Hali hii inaongeza tishio na hatari ya maambukizi ya Virusi vya ugonjwa wa Polio katika Mkoa wetu

ikizingatiwa kuwa watoto tisa kati ya kumi wenye maambukizi ya Ugonjwa wa Polio huwa hawaoneshi dalili. Aidha Mgonjwa mmoja kati ya watoto mia mbili wenye maambukizi hupata ulemavu wa kudumu.

Ndugu Washiriki, Kutokana na tishio lililotajwa hapo juu pamoja na ukaribu wa kijiografia na mwingiliano mkubwa wa watu uliopo kati ya Mkoa wetu na nchi zenye Mlipuko wa ugonjwa wa Polio hivi sasa, napenda nichukue fursa hii kuwataarifu kuwa tutakuwa na Kampeni maalum ya utoaji wa chanjo ya matone dhidi ya Polio kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka nane (8). Kampeni hii itafanyika kwa siku nne (4) kuanzia tarehe 21 – 24 Septemba, 2023 katika Mkoa wetu pamoja na mikoa sita (6) inayopakana na nchi zenye mlipuko wa Polio ambayo ni Kagera, Kigoma, Katavi, Songwe na Mbeya.

Ndugu Washiriki, Lengo la kampeni hii ni kuwafikia watoto 391,883 waliozaliwa baada ya mwaka 2016 ili kuwakinga dhidi ya Kirusi cha Polio aina ya pili (Polio Virus Type 2) kinachoweza kusababisha ulemavu wa kudumu. Kwa Halmashauri ya Manispaaa ya Sumbawanga tunatarajia kufikia watoto 83,881, Sumbawanga vijijini 118,071, Kalambo 80,486 na Nkasi 109,514.

Ndugu Washiriki, Ili kufanikisha Kampeni hii, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Wadau wa chanjo imeshafanya maandalizi kwa ajili ya kuwezesha zoezi hili kuendeshwa bila kuathiri shughuli nyingine za wananchi. Aidha, wakati wa Kampeni kutakuwa na timu yenye jumla ya watoa huduma za afya 1,038 kwa Mkoa wa Rukwa ambapo kila timu itakuwa na watoa huduma watatu. Timu hizi zitakuwa zinatoa huduma ya chanjo kwa walengwa kupitia vituo vya kutolea huduma za afya, nyumba kwa nyumba, shuleni na

maeneo mbalimbali ya mikusanyiko ikiwemo Nyumba za Ibada.

Ndugu Washiriki, Natumia fursa hii kutoa maelekezo kwa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya zote za Mkoa wa Rukwa usimamia kwa karibu maandalizi na utekelezaji wa kampeni hii kupitia Kamati za Afya ya Msingi ngazi za Wilaya. Aidha, awaelekeza Waganga Wakuu wa Halmashauri kuhakikisha upatikanaji wa chanjo, vifaa na mafunzo kwa wataalam atakaohusika katika utoaji wa chanjo. Aidha, ninaelekeza kuimarisha afua za utoaji wa elimu kwa umma kuhusu ugonjwa wa Polio na chanjo hii kwa kutumia njia mbalimbali na kwa kuzingatia mazingira mahususi ya eneo husika.

Ndugu Washiriki, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inawahimiza wananchi kuendelea kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya Ugonjwa wa Polio kama inavyoshauriwa na wataalam wa afya kwa kufanya yafuatayo: Kuwahi katika kituo cha kutolea huduma za afya mapema kwa ajili ya uchunguzi na matibabu mara tu unapoona dalili za kupooza kwa ghafla; Kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono ili kujikinga na magonjwa mbalimbali ya kuambukiza; Kuhakikisha matumizi sahihi ya vyoo bora wakati wote; na Kuhakikisha watoto wote wanapata chanjo kulingana na ratiba ili kuwakinga dhidi ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo.

Mwisho, nitoe rai kwa wazazi na walezi kutoa ushirikiano kwa watoa huduma za afya ili kuwezesha watoto wao kuchanjwa kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba. Baada ya maelezo haya napenda kutamka kuwa kikao cha Kamati ya Afya ya Msingi ngazi ya Mkoa kimefunguliwa rasmi.

Mungu Ibariki Tanzania,
Mungu Ubariki Mkoa wetu wa Rukwa,

Asanteni kwa kunisikiliza.

Charles Makongoro Nyerere
MKUU WA MKOA RUKWA.